Australian Government

Department of Immigration and Citizenship

Habari za makazi kwa wahamiaji nchini Australia

Form
994i SWA
SWAHILI

Hongera kwa uamuzi wako kuhamia Australia. Tunakutakia kila la heri na tunatumaini utafurahia kuwa katika nchi yako mpya.

Fomu hii hutoa muhtasari mfupi wa mambo muhimu kadhaa ambayo unafaa ufikirie unapojiandaa kwa maisha mapya yako nchini Australia na inapatikana katika tovuti ya Idara ya Uhamiaji na Uraia (idara yenyewe) kwa Kiingereza na lugha 37 katika **www.immi.gov.au/allforms/languages/languages_num.htm** Kwa wahamiaji wengi vyanzo vya kwanza vya habari kuhusu Australia ni ndugu, marafiki na wahusika nchini Australia. Utafiti wowote wa ziada unaoweza kufanywa kabla ya kuwasili utakusaidia matarajio ya makazi yako.

Gombo za tovuti za *Kuishi nchini Australia* za idara zinapatikana kutoka **www.immi.gov.au/living-in-australia/** na hutoa ujumbe wa makazi wa habari zaidi pamoja na huduma zinazopatikana kwa wahamiaji wapya waliowasili.

Vijitabu vya *Kuanza maisha nchini Australia* vinapatikana katika Kiingereza na lugha 37 za kijamii. Vina habari nyingi ndani kuhusu huduma kwa wahamiaji wanaotazamiwa na wapya wanaowasili, na vinapatikana kutoka **www.immi.gov.au/living-in-australia/settle-in-australia/beginning-life/**

Jamii anuwai ya Australia

Australia ni jamii anuwai inayopokea na iliyo na watu kutoka asili nyingi tofauti za kitamaduni, kikabila, kilugha na kidini. Waaustralia wametoka pembe zote za ulimwengu. Takribani 44% ya Waaustralia walizaliwa ng'ambo au wana mzazi aliyezaliwa ng'ambo.

Waaustralia wanafuata dini anuwai nyingi. Kila mtu yuko huru kuonyesha na kudumisha desturi zao za kitamaduni na kidini, chini ya sheria, na wanaweza kuhusika na kujumuika kama Mwaustralia. Mwanzoni, unaweza kuwa hujazoea anuwai kama hiyo lakini ukiwa wazi na unaonyesha heshima kwa watu, mawazo na desturi, unaelekea kuingiliana nao na kufaulu katika maisha yako mapya.

Uhuru na usawa tunaofurahia nchini Australia unategemea kila mtu kutimiza majukumu yake. Unatarajiwa uwe mwaminifu kwa Australia, uunge mkono njia yetu ya maisha ya kidemokrasia na usaidie kuendeleza desturi za Australia za kukubali, kuwa wote pamoja na usawa kwa wote. Kuna sheria za shirikisho, jimbo na wilaya zinazokataza ubaguzi kwa sababu mbalimbali (kwa mfano umbari, jinsia, ulemavu, umri au upendeleo wa ujinsia) na katika maeneo mbalimbali ya umma (kwa mfano ajira, elimu, malazi, kupata bidhaa na huduma, na vitendo vya serikali).

Kiingereza ni lugha ya taifa, ingawa kuna zaidi ya lugha 260 zinazozungumzwa nchini Australia, pamoja na lugha za asili. Kama huwezi kusema Kiingereza tunakuhimiza sana ujifunze haraka iwezekanavyo baada ya kuwasili. Labda utastahili kupokea masomo ya bure kupitia Mpango wa Kiingereza kwa Wahamiaji Ngumbaru (AMEP). Habari kuhusu mpango huu zipo kwenye ukarasa wa 5.

Forodha na karantini

Ubalozi wa Australia unaweza kukupa ujumbe kuhusu kanuni za forodha na karantini. Itakufahamisha vitu gani unaweza au huwezi kuvileta nchini Australia, hali maalum za kuyaleta matumizi ya nyumbani, wanyama/bidhaa vilivyotengenezwa kutokana na wanyama, na juu ya ushuru wa forodha. Kwa habari zaidi enda kwa www.customs.gov.au

Fedha na benki

Tayarisha hundi za wasafiri au fedha zinazokubalika nyingine, kwa mfano dola za US au Australia kabla ya kusafiri. Unaweza kubadilisha fedha za kigeni kuwa dola za Australia kwenye viwanja vingi vya ndege vya kimataifa vya Australia.

Kwa kawaida watu huweka pesa zao kwenye benki au taasisi nyingine za kifedha. Ukifungua akaunti kwa mojawapo ya taasisi hizi kati ya wiki 6 baada ya kuwasili kwako, kawaida unahitaji pasipoti tu. Baada ya wiki 6 utahitaji kitambulisho cha ziada ili kufungua akaunti.

Usafiri

Utahitaji kutafuta usafiri kutoka kiwanja cha ndege kufikia malazi yako. Kuna teksi na mabasi kwenye viwanja vyote vya ndege vya kimataifa na viwanja vingi vingine vya ndege.

Ili kuendesha gari, unahitaji leseni ya dereva wa Australia. Leseni ya dereva ya kimataifa inaweza kutumika kwa muda mfupi. Wasiliana na idara ya usafiri iliyo karibu zaidi ya jimbo au wilaya kwa habari kuhusu kupata leseni ya dereva. Saraka ya simu za mitaa inaorodhesha shirika linalofaa na namna ya kuwasiliana nao.

Kutotii sheria za barabarani kunaweza kusabisha kutokea kwa faini yenye gharama kubwa, kupoteza leseni ya dereva au hata kufungwa jela. Sheria nchini Australia ni kali kuhusu kikomo rasmi cha spidi na kuendesha baada ya kunywa pombe. Ni hatia kunywa pombe au kulevya unapoendesha. Sheria ya Australia inasema kwamba kila mtu anayesafiri katika gari lazima atumie mkanda wa kiti au kitasi kumfunga mtoto.

Makao

Kupanga/kununua nyumba/gorofa, unaweza kutafuta na kuipata kupitia matangazo kwenye magazeti, mtandaoni au kwa ajenti wa shirika la nyumba. Malipo ya dhamana, sawa na kiwango cha kodi ya mwezi, pamoja na kodi ya mwezi mmoja mapema ni kawaida unapopanga. Kupata makao nchini Australia yaweza kuwa vigumu na kodi yaweza kuwa ghali.

Shule

Kwenda shuleni ni lazima kwa watoto wote wenye umri kati ya miaka 5 na 15. Umri huu unabadilika kidogo kwa baadhi ya majimbo na wilaya. Unapaswa kuwaandikisha watoto shuleni kwa haraka iwezekanavyo.

Shule za mapema zinapatikana pia kwa watoto wenye umri kati ya miaka 3 na 5. Kawaida ni ya muda maalum na sio lazima.

Habari za shule za mitaa zinapatikana kutoka idara za elimu ya jimbo au wilaya. Saraka ya simu ya mitaa hutoa habari za mawasiliano.

Usalama nchini Australia

Kama katika nchi yoyote, kunazo hatari za kuepukwa. Kuogelea baharini au mitoni kunaweza kuwa hatari sana na hata ikatishia uhai. Katika pwani wa bahari, unafaa kuogelee kati ya bendera nyekundu na ya manjano au usiogelee kabisa. Kuvua samaki kwenye mawe ya bahari pia ni hatari sana.

'Msitu' wa Australia unao nyoka na wadudu hatari. Katika miji mikubwa unafaa uwe mwangilifu kuhusu usalama wako wa kibinafsi wakati wa usiku sana.

© COMMONWEALTH OF AUSTRALIA, 2011

Gharama ya kuishi nchini Australia

Gharama ya kuishi nchini Australia ni ya juu, kulinganisha na nchi zingine nyingi. Ni lazima ufikirie utakavyopata mahitaji yako na ya familia yako kwa muda usiopungua miaka 2 ya kwanza. Usisadiki kwamba utapata kazi haraka.

Gharama ya kuhamia ni kubwa. Kuna gharama muhimu kuhusika unaposafiri kwenda Australia, kusafirisha vifaa vya nyumbani pamoja na kuanzisha maisha mapya katika nchi nyingine.

Malipo na huduma za Centrelink

Serikali ya Australia inatoa huduma ili kuwasaidia watu kujitegemea na kusaidia wale wanaohitaji kusaidiwa kupitia shirika liitwalo Centelink.

Maelezo yanayotolewa hapa ni mwongozo wa kijumla tu na ni lazima uzungumze mahitaji yako maalum na Vituo vya Huduma vya Centrelink.

Unaweza kuzipata Vituo vya Huduma vya Centrelink na nambari zao za simu katika saraka ya simu ya mtaa. Unaweza kuongea nao wafanyakazi wa Centrelink na kupata majibu kwa maswali yako katika lugha zingine kando ya Kiingereza ukipiga simu 131 202. Hii si huduma ya mkalimani. Simu za nambari hii zinalipishwa kwa gharama ya simu ya mtaa kutoka popote Australia. Kutumia simu za kulipiwa za umma au simu za mkononi zaweza kutozwa kiwango cha juu zaidi.

Centrelink ina maelezo mengi kuhusu huduma na malipo yake pamoja na ujumbe uliotafsiriwa anuwai kubwa. Kwa maelezo zaidi kuhusu machapisho yaliyotafsiriwa ya Centrelink, piga simu 131 202 au angalia tovuti www.centrelink.gov.au na chagua 'Tunaongea lugha yako' kwa ukurasa wa tovuti wa Centrelink.

Maelezo zaidi kuhusu malipo ya ruzuku ya serikali au makubaliano ya kitaifa kabla ya kuwasili Australia yanapatikana katika:

Tovuti: www.centrelink.gov.au

Posta: Centrelink International Services
GPO Box 273
HOBART TAS 7001
AUSTRALIA

Simu: 131 673 (Huduma za Kimataifa za Centrelink nchini Australia)
131 202 (kwa maelezo katika lugha zingine kando ya Kiingereza)
+613 6222 3455 (nje Australia)
(**Ukumbusho**: Ukitaka kupigia simu Huduma za Mataifa za Centrelink kutoka nje ya Australia, nambari za simu ya bure zinapatikana kwenye nchi nyingi. Angalia tovuti ya Centrelink kwa orodha ya nambari hizi.)

Malipo ya familia

Hakuna muda wa kusubiri kwa malipo ya familia yanayosaidia na gharama ya kuwalea watoto. Wahamiaji pia wanaweza kupata utunzaji wa afya mara moja chini ya Medicare Australia.

Huduma za Msaada wa Familia zinapatikana katika ofisi zote za Medicare na Centrelink. Maelezo zaidi pamoja na karatasi za maelezo za lugha nyingi yanapatikana kutoka:

Tovuti: www.familyassist.gov.au

Simu: 136 150 (nchini Australia)
131 202 (kwa maelezo katika lugha zingine kando ya Kiingereza)

Maelezo ya kijumla ya elimu ya utoto mdogo na huduma ya kutunza watoto yanapatikana kutoka:

Tovuti: www.mychild.gov.au

Simu: 133 684 (nchini Australia)

Muda wa Kusubiri wa Wakazi Waliowasili Karibu

Kama wewe ni mhamiaji mpya katika Australia kwa kawaida huwezi kupata ruzuku mara moja kutoka Centrelink.

Kama mkazi aliyewasili karibu, unapaswa kwa kawaida kusubiri wiki 104 (Muda wa Kusubiri wa Wakazi Waliowasili Karibu) kabla ya kuweza kupata malipo mengi na faida nyingi kama Posho ya Newstart au Posho ya Vijana.

Urefu wake, jinsi inavyohesibiwa na anayehusika inategemea uwasili wako nchini Australia na ruzuku unayoomba. Muda uliokaa Australia kama mkazi wa Australia kwa wakati wowote katika maisha yako unaweza kuhesibiwa katika muda wa kusubiri.

Kama unaathiriwa na Muda wa Kusubiri wa Wakazi Waliowasili Karibu ni muhimu kuwasiliana na Centrelink mara moja kama hali yako inabadilika, kwa mfano ukipata mtoto, ukipoteza kazi au ukigonjeka.

Buraa ya Muda wa Kusubiri wa Wakazi Waliowasili Karibu

Kuna msamaha kadhaa kutoka Muda wa Kusubiri wa Wakazi Waliowasili Karibu pamoja na kama wewe ni raia wa Australia au ndugu wa raia wa Australia, mtu aliyewasili katika mradi wa ukimbizi au wa huruma au ni mmiliki wa aina fulani ya viza.

Kama ukipata mateso kwa sababu ya mabadiliko makubwa ya hali usiyoweza kuzuia, unaweza kustahiki Faida Maalum. Kupoteza au kutoweza kupata kazi kwa kawaida haitambulika kama kuwa mabadiliko ya hali.

Kuna sababu za ziada zinazosamehe watu wengine kusubiri muda ule kwa ruzuku fulani. Unafaa uwasilishe ombi na Centrelink ili wapime kama unastahiki buraa au la.

Sharti la Kustahili Ukazi

Pensheni na ruzuku zingine hazina muda wa Kusubiri wa Wakazi Waliowasili Karibu, lakini zina masharti ya 'kustahili makazi'

1. Ruzuku ya Uzazi na Posho ya Mjane zina masharti ya kustahili makazi ya wiki 104.
2. Pensheni ya Uzee na Pensheni ya Kusaidia Ulemavu zina masharti ya kustahili makazi ya miaka 10.

Kuna buraa ya masharti hayo, kwa mfano, kama wewe ni mkimbizi, ukiwa mlemavu baada ya kuwasili nchini Australia, au umetoka nchi ambayo ina mapatano ya ruzuku na Australia na mapatano yanayohusika malipo unayoomba.

Raia wa New Zealand (ambao si raia wa Australia)

Watu wanaowasili nchini Australia kwa kutumia pasi la New Zealand kwa kawaida wanapewa Viza ya Aina Maalum (SCV) wanapowasili. Wenye kumiliki SCV ambao walikuwepo Australia tarehe 26 Februari 2001 kwa kawaida wanatambuliwa kama kuwa wenye SCV Kulindwa. Wale waliowasili nchini Australia baada ya 26 Februari 2001 wanatambuliwa kuwa Kutolindwa.

Wenye SCV Kulindwa wanastahiki kuwa wakazi wa Australia na kawaida wanaweza kupata malipo yote ya Centrelink wakikaa Australia sasa na wakitosheleza masharti fulani kama vigezo vya kustahili na muda wa kusubiri unaofaa.

Wenye pasi ya New Zealand ambao wamekaa nchini Australia endelevu kwa angalau miaka 10 tangu tarehe 26 Februari 2001 na wanao SCV kutolindwa labda wataweza kupata malipo mara moja tu ya Posho wa Newstart, Posho ya Ugonjwa au Posho wa Vijana. Ukistahili, malipo yanaweza kufanywa kwa muda endelevu wa mwisho wa miezi 6.

© COMMONWEALTH OF AUSTRALIA, 2011

Mapatano ya Ruzuku kati Australia na New Zealand unaweza kuwasaidia raia wengine wa New Zealand kulipiwa Pensheni wa Uzee, Pensheni ya Msaada wa Ulemavu au Ruzuku ya Mtunzaji.

Wenye pasi ya New Zealand wanaokaa Australia wanaweza kustahili kadi fulani ya ruzuku baada ya muda wa kusubiri na malipo kutoka Ofisi ya Msaada wa Familia.

Uhakika wa Msaada

Uhakika wa Msaada ni mapatano ya kisheria kwa na Mkazi wa Australia au shirika (mwenye uhakika) na Serikali ya Australia. Mwenye hakika anakubali kutoa msaada kwa mhamiaji (mpokeaji uhakika) nchini Australia ili mpokeaji uhakika hahitaji kutegemea ruzuku ya Centrelink. Uhakika wa Msaada unaweza kuendelea kwa miaka 2 au 10, kutegemea aina ya viza inayotolewa. Kama wewe au wale wanaokutegemea wanaomba malipo fulani kutoka Centrelink wakati wa mapatano wa Uhakika wa Msaada, mwenye hakika apaswe kulipa tena kiasi kizima kwa serikali.

Afya

Serikali ya Australia hutoa msaada wa gharama za uganga, miwani matibabu na huduma ya hospitali kupitia mradi unaoitwa Medicare. Medicare hutoa matibabu ya bure ukiwa mgonjwa (wa Medicare) wa serikali katika hospitali ya serikali na matibabu ya bure au yenye gharama ya chini yanayotolewa na wataalum kama madaktari, bingwa, madaktari wa miwani na wa meno wanaoshirki (huduma zilizotajwa tu). Ukifika mpaka wa Wavu ya Usalama wa Medicare, kumwona daktari wako au kupata mapimo yanaweza pia kukugharimu gharama ya chini zaidi.

Ili kujua kama unastahiki Medicare, na kuijiandikisha na Medicare, tembelea ofisi ya Medicare Australia ya eneo lako, na pasipoti yako, hati ya kusafiria na viza yako ya kudumu. Kama bado hujapata viza ya hiyo kudumu, pia utahitaji kutoa habari za maombi yoyote ya kuhamia au kupata viza ya kudumu ambayo umewasilisha.

Wengi wenye viza ya muda hawastahiki kujiandikisha na Medicare, lakini kuna buraa kadhaa, kwa mfano watu ambao wameomba viza ya kudumu na wameshakubali vigezo vinavyohitajika. Utembelee ofisi ya Medicare ya eneo lako kujua ukistahiki Medicare. Ukifikia mahitaji yote ya kistahiki, utaweza kupewa namba yako ya kadi ya Medicare ya muda kutumia mpaka kadi yako inafika kwa posta yamkini wiki 3. Katika visa vingi, utalipia huduma ya matibabu kisha utarudishiwa faida kutoka Medicare.

Serikali ya Australia pia husaidia na gharama ya madawa mengine chini ya Mpango wa Fadhila ya Madawa (PBS). Ukihitaji madawa mengi katika mwaka mmoja, Wavu ya Usalama ya PBS inaweza kukusaidia. Unapofika Wavu ya Usalama ya PBS, na mkemia amekupa kadi ya Wavu ya Usalama ya PBS, madawa yako ya PBS yatakuwa na gharama chini au bure kwa muda unaobaki wa mwaka. Ukichagua aina ya dawa ya gharama juu zaidi au daktari yako anakuagiza hivi, unaweza kulipa zaidi.

Medicare na PBS zinasimamiwa na Medicare Australia.

Medicare Australia inasimamia Rejesta ya Mchanjo Utotoni ya Australia, rejesta inayoweka kumbukumbu ya habari za mchanjo uliowapa watoto chini wa umri wa miaka 7. Ukiwa na mtoto mwenye umri chini ya miaka 7, tafadhali hakikisha ulete rekodi zao za uchanjaji kumsaidia daktari wako nchini Australia kuamua kama uchanjaji wao unatosheleza. Kumbukumbu ya mchanjo wa mtoto wako itakusaidia kutosheleza mahitaji ya mchanjo unapomwandikisha watoto wako shuleni na pia hilo ni sharti la baadhi ya malipo ya Msaada wa Familia.

Medicare Australia inatekeleza Rejesta ya Mdhamini wa Sehemu ya Mwili ya Australia (Rejesta ya Mdhamini). Watu wenye umri zaidi ya miaka 16 wanaweza kusajili uamuzi wao unaohusu mchango wa viungo au tishu vya mwili kwenye Rejesta ya Mdhamini. Kuweka kumbukumbu za uamuzi wako kwenye Rejesta ya Mdhamini ni hiari na unaweza kuchagua viungo vipi na tishu ipi utataka kutoa. Kwa watu wenye ugonjwa wa hatari au wa kutisha uhai, kuhamisha sehemu ya mwili au tishu kunaweza kumaanisha mianya ya pili kuishi.

Medicare Australia pia inatekeleza Mpango wa Meno ya Ujana wa Medicare. Mpango wa Meno ya Ujana wa Medicare husaidia watu wa ujana, walio nao umri wa miaka 12 hadi 17, wanaostahiki na gharama ya meno kuangaliwa ya kuzuia cha kila mwaka. Kama ukistahiki, barua na vocha itatumwa kwako. Uchunguzi wa meno wa kuzuia inaweza kuwa pamoja na eksrai, kupaa na kusafisha meno, matibabu ya msombo, mafunzo ya usafi wa mdomo, ushauri wa chakula na kujaza mashimo na ufa wa meno.

Medicare ina chombo cha habari kinachotafsiriwa katika lugha 19. Chombo kina ujumbe kuhusu mipango na huduma za Medicare Australia na inafafanua mahitaji ya kustahiki fadhila na malipo. Nakala za paketi zinapatikana kutoka tovuti ya Medicare Australia au ofisi ya Medicare ya eneo lako.

Kwa habari zaidi:

Tovuti:	www.medicareaustralia.gov.au	
Baruapepe:	info@medicareaustralia.gov.au	
Simu:	132 011*	– Medicare
	1800 020 613**	– Mpango wa Fadhila ya Madawa
	1800 653 809**	– Rejesta ya Uchanjaji wa Utoto ya Australia
	1800 777 203**	– Rejesta ya Mdhamini wa Sehemu ya Mwili ya Australia
	1800 552 152**	– Kwa walemavu wa kusikia na kunena
	131 450*	– Huduma ya Utafsiri na Ukalimani
Posta:	Medicare Australia GPO Box 9822 Kwa mji mkuu wako	

Bima ya afya ya kibinafsi

Waaustralia wengi wanachagua kuchukua bima ya afya ya kibinafsi. Hushughulikia gharama ya matibabu kadhaa au yote kama mgonjwa wa kibinafsi katika hospitali ya binafsi au ya umma, na inaweza ikajumuisha huduma zingine ambazo Medicare haitoi, kama vile huduma za meno, huduma nyingi za macho na usafiri wa ambulensi. Ukifikiria kuchukua bima ya afya ya kibinafsi ufahamu zifuatazo:

1. Kipunguo cha Bima cha Afya ya Kibinafsi – Unaweza kustahiki kudai Kipunguo cha Bima cha Afya ya Kibinafsi ukiwa unastahiki Medicare na una hati ya bima ya afya yenye ridhaa inayotoa bima ya matibabu ya hospitali, matibabu ya jumla ('ziada') au yote mawili.
2. Mchango wa Kodi ya Medicare – Waaustralia wengi ambao wanalipa kodi wana Kodi ya Medicare pamoja na kiwango cha kodi wanayolipa. Mchango wa Kodi ya Medicare ni malipo ya ziada unayotozwa watu wanaopata ajira kupita kiwango cha juu cha mshahara fulani na hawana bima ya hospitali ya kibinafsi. Kiwango cha juu cha mapato ni (katika mwaka wa kipesa wa 2011-12) dola AUD80,000 kwa mwaka kwa mtu moja na dola AUD160,000 kwa mwaka kwa mume na mke au familia. Viwango hivi vitabadilishwa kila mwakani kulingana na mabadilisho ya mishahara ya wastani.

* Simu zinatozwa

** Simu zinatozwa kutoka simu za mkononi au za kulipia tu

© COMMONWEALTH OF AUSTRALIA, 2011

3. Bima ya Afya ya Maisha – Bima ya Afya ya Maisha (LHC) ni upakaji wa kifedha unaoweza kujumlisha na malipo ya msingi kwa bima ya hospitali ya afya ya binafsi. Ili kuepuka upakaji wa bima (LHC), lazima ununue bima ya hospitali kutoka kwa mwenye bima ya Australia iliyoandikishwa kabla ya mpaka wako wa mwisho wa bima (LHC). Mpaka wa mwisho kawaida huwa ni tarehe 1 Julai inayofuata sikukuu yako ya kuzaliwa ya umri wa miaka 31, lakini ukiwa mhamiaji mpya nchini Australia mpaka wako wa mwisho wa bima ya afya ya maisha waweza kuwa baadaye, kutegemea umri wako ulipowasili nchini Australia.

   Ukinunua bima ya hospitali baada ya mpaka wako wa mwisho labda utahitajika kulipa upakaji wa bima ya afya ya maisha (LHC) - kiasi cha asilimia 2% zaidi juu ya malipo yako ya kila mwaka umri wako unapozidisha miaka 30 wakati unapoanza na bima. Kwa mfano, ukingoja mpaka unapofikisha miaka 40, ungeweza kulipa 20% zaidi ya gharama ya bima yako ya hospitali.

   Wahamiaji wapya wanaowasili Australia ambao wapo tayari na umri juu wa 31 hawalipi gharama zaidi wakinunua bima ya afya ya kibinafsi kati ya miezi 12 kuanzia siku waliyojiandikisha kustahiki ruzuku mzima za Medicare. Ni muhimu kufikiria kuchukua bima ya hospitali katika mwaka wako wa kwanza baada ya kujiandikisha Medicare. Ukichagua kusubiri zaidi kuliko miezi 12 baada ya kujiandikisha Medicare, kisha labda utahitajika kulipa upakaji ya Bima ya Afya ya Maisha (LHC) kujumlisha malipo yako. Ukiwa chini ya umri wa miaka 31 unapowasili nchini Australia, basi mpaka wako wa mwisho wa bima (LHC) utakuwa sawa na wa watu mwengineo (Julai 1 inayofuatia sikukuu yako ya kuzaliwa ya 31).

Habari zaidi kuhusu bima ya afya ya kibinafsi inapatikana katika:

Tovuti: www.privatehealth.gov.au

Baruapepe: privatehealth@health.gov.au

Posta: MDP 954
Department of Health and Ageing
GPO Box 9848
CANBERRA ACT 2601
AUSTRALIA

Ajira nchini Australia

Soko la ajira Australia ni ya mashindano. Ajira katika Australia inategemea vipengele vya kichumi, aina ya kazi inayotafutwa na hali maalum inayoweza kuathiri upatikanaji wa kazi sehemu mbalimbali nchini. **Kukubaliwa kuhamia haihakikishi kazi,** hata kwa waombaji waliotathminiwa kuwa na ustadi juu.

Kwa Mai 2011, kiwango cha mwelekeo wa kukosa ajira nchini Australia kilikuwa 4.9%. Wahamiaji waliozaliwa nchi za kuzungumza Kiingereza walikuwa na kiwango cha kutoajiriwa cha 4.1%, wakati waliozaliwa nchi nyingine walikuwa na kiwango cha 6.1%. Wahamiaji waliowasili tangu mwaka wa 2006 walikuwa na kiwango cha kukadiria kukosa ajira cha 7.6% (takwimu). Kwa jumla, wahamiaji ambao wamekuwa na nafasi zaidi kutulia Australia wanakuwa na viwango vya kutoajiriwa chini zaidi. Vivyo hivyo, wale wanaoingia Australia chini ya Ustadi Kuu wana viwango vya kutoajiriwa chini zaidi kuliko wale wanaoingia chini ya aina nyingine.

Kujua kuhusu matarajio ya kazi yako, soma magazeti ya Australia yanayoorodhesha nafasi za kazi. Pia kuna tovuti nyingi mtandoni za uandikishaji.

Kabla ya kuhamia Australia uchunguze kama kuna mahitaji au masharti yoyote yanayohusu kazi unazotaka kufanya. Kwa kazi nyingi nchini Australia, waombaji wapaswa kuweza kujiandikisha au kupata leseni na mamlaka ya jimbo au wilaya ya Australia, na/au kustahiki kwa uanachama wa shirika la bingwa au tasnia.

Uchunguze kama mahitaji yoyote ya kuandikisha au kupata lesensi yanatumika kazi yako. Wanaotegemea wafanye maulizo hayohayo kuhusu matarajio ya kazi zao, wakikusudia, au sivyo, kutafuta kazi mara moja baada ya kuwasili.

Wahamiaji wasio na kazi wajiandikishe na Centrelink haraka wawezavyo baada ya kuwasili. Kwa sababu wahamiaji wengi waliowasili wapya kwa jumla hawastahiki malipo ya mapato kwa wiki 104, wanaweza kustahiki kutia maombi ya huduma za msaada wa kutafuta kazi anuwai kidogo zilizofadhiliwa na serikali kupitia Huduma za Kazi Australia. Hata hivyo, wahamiaji ambao ni wakazi wa kudumu na wanapata vigezo vingine vya ustahiki wanaweza kustahiki kutia maombi ya anuwai yote kupitia Huduma za Kazi Australia.

Habari za huduma za ajira, kutafuta kazi na kutambua hitimu unapatikana katika tovuti zifuatazo:

- KutafutaKazi Australia (kwa habari kuhusu kazi, utarajio wa ajira, uhaba wa ustadi na amali katika Australia) www.jobsearch.gov.au
- Mahali pa Kazi ya Australia (kwa habari za mahali pa kazi ya Australia) www.deewr.gov.au
- Kutambua Utaalamu Australia (kwa kutambua hitimu za utaalamu) www.deewr.gov.au/tra
- Habari za Kutambua Ustadi wa Australia (kwa kutambua hitimu na ustadi za ng'ambo) **www.immi.gov.au/asri**

Ushuru/Kodi nchini Australia

Nchini Australia, ushuru/kodi hutolewa kutoka fedha unazopata kutoka kazi, biashara au kitega uchumi.

Ofisi ya Ushuru ya Australia inakusanya ushuru kutoka watu na biashara kulipa kwa huduma muhimu za jamii kama hospitali, mashule, barabara na reli.

Ushuru na watu

Ukiwa unafanya kazi, mwajiri wako anatoa ushuru mwenyewe kutoka mshahara au ujira wako. Mwisho wa kila mwaka wa kifedha, uwasilishe fomu ya kurudisha ushuru na Ofisi ya Ushuru inayoonyesha kiasi ulichopata na kiasi cha ushuru kilichotolewa na kipato chako. Waweza kupunguza kiasi cha ushuru kwa kudai vipunguzo na fidia kadhaa vya ushuru.

Kabla ya kuanza kufanya kazi, unafaa kutia ombi la Nambari ya Faili ya Ushuru (TFN) kutoka Ofisi ya Ushuru. TFN ni nambari ya kipekee inayopewa watu na mashirika kwa sababu ya kitambulisho na kutunza makumbusho. Usipokuwa na TFN, lazima mwajiri wako atoe kiasi cha mwisho cha ushuru kutoka mapato unayopewa. Ni muhimu uhifadhi TFN yako. Kuruhusu mwengine kutumia TFN yako, kuiuza au kumpa mwengine kunaweza kusabibisha matatizo makubwa kwako.

Ushuru na biashara

Ukifikiri kuendesha biashara nchini Australia, utahitaji TFN na Nambari ya Biashara ya Australia. Pia utahitaji kujiandikisha kwa Ushuru ya Bidhaa na Huduma (GST) kama mapato na matumizi yako yanazidi dola AUD75,000. Utahitaji kulipa ushuru ya mapato ya biashara yako na labda utahitaji kulipa ushuru kwenye faida ya mali unayopata ukiuza biashara au mali yako.

Sheria ya Australia pia inahitajika ulipe fedha katika akaunti ya malipo ya uzeeni kwa kila mtu unayeajiri na kwamba utoe ushuru kutoka mapato ya wajira wako na kuituma kwa Ofisi ya Ushuru.

© COMMONWEALTH OF AUSTRALIA, 2011

Maelezo zaidi

Kusaidia biashara na watu kuelewa haki na majukumu yao ya ushuru, Ofisi ya Ushuru inatoa bidhaa anuwai ya msaada. Hii ni pamoja na machapisho ya Kiingereza na ya lugha nyingine, semina, habari za tovuti na kutembelea uso-kwa-uso. Ofisi ya Ushuru imetunga maonyesha bure yaitayo 'Ushuru nchini Australia – unachohitaji kujua' inayopatikana kama DVD au kwa intanet. 'Ushuru nchini Austalia' inatoa maelezo ya msingi kuhusu mfumo wa ushuru, TFNs, kuwasilisha ushuru/kodi na zaidi. Inapatikana katika lugha 15 pamoja na Kiingereza.

Kwa habari zaidi:

Tovuti: www.ato.gov.au

Simu: 132 861 (katika Australia)

Baruapepe: diversity@ato.gov.au

Huduma za Makazi ya Wahamiaji

Idara ya Uhamiaji na Uraia hufadhili huduma za makazi anuwai zinazolenga kusaidia wahamiaji na washiriki wa huruma kuwa wahusika wazuri katika jamii ya Australia kwa haraka iwezekanavyo baada ya kuwasili.

Mpango wa Ruzuku ya Makazi

Mpango wa Ruzuku ya Makazi (SGP) unalenga kuwasaidia wahamiaji na wakimbizi wanaostahiki kuweza kujitegemea na kuhusika kwa sawa katika jamii ya Australia mapema iwezekanavyo baada ya kuwasili.

Idara ya Uhamiaji na Uraia kupitia Mpango wa Ruzuku ya Makazi unafadhili mashirika yasiyo ya kibiashara pamoja na mashirika yanayotoa huduma ya kiserikali yanahutoa usaidizi wa makazi kwa wateja wanaostahiki.

Unaweza kufikia huduma za Mpango wa Ruzuku ya Makazi kama wewe ni mkazi wa kudumu na umewasili nchini Australia katika miaka mitano iliyopita kama:

- mshiriki wa huruma;
- mhamiaji wa mtiririko wa familia aliye na ustadi mdogo wa Kiingereza;
- watu wanaotegemea wahamiaji wenye ustadi wa eneo la shambani au mkoani ambao wana ustadi mdogo wa Kiingereza.

Baadhi ya wakazi wa muda (wenye viza ya Kutazamia Ndoa, Mwenzi ya Muda, Mume/Mke wa Muda na Kutegemeana kwa Muda pamoja na wanaotegemea) katika maeneo ya shambani na mkoani waliokuwa na ustadi mdogo wa Kiingereza pia wanastahiki huduma za Mpango wa Ruzuku wa Makazi.

Watoa huduma ya Mpango wa Ruzuku ya Makazi wanaweza kukutolea habari kuhusu njia za kufika huduma za kawaida kwa mfano makazi, huduma ya watoto, kazi na elimu shuleni. Pia wanaweza kukusaidia kuunganisha na mtandao wa msaada unaoweza kukusaidia kutulia katika jamii.

Unaweza kuipata orodha ya watoa huduma za makazi inapatikana kutoka **www.immi.gov.au/living-in-australia/settle-in-australia/find-help/where-to-help/**

Mpango wa Kiingereza kwa Wahamiaji Ngumbaru

Kujifunza Kiingereza ni hatua mmojawapo na muhimu sana unayoweza kuchukua kuelekea kufaulu kutulia nchini Australia na kutimiza malengo yako ya kibinafsi, kijamii na kiuchumi. Ukistahiki, Mpango wa Kiingereza kwa Wahamiaji Ngumbaru (AMEP) unaweza kutoa mafunzo bure ya lugha ya Kiingereza ya msingi yatakayokusaidia kujimudu hali ya kijamii ya kawaida na hali ya kazi kadhaa.

Ukistahiki msaada wa AMEP, unaweza kujifunza Kiingereza hadi masaa 510, au mpaka utakapofika Kiingereza kinachofaa, yoyote inayofika kwanza. Ukiwa mshindani wa huruma ambaye amepita matukio magumu kama mateso au kiwewe kabla kuwasili Australia, au kama ulipata kiasi kidogo cha elimu shuleni, labda utaweza kupokea masomo zaidi ya Kiingereza.

Lazima ujisajili kwa masomo ya AMEP na mtoa huduma ya AMEP katika eneo lako ndani ya miezi 6 ya kuwasili nchini Australia au kupata makazi ya kudumu. Lazima uanze madarasa karibu uwezekanavyo ndani ya mwaka mmoja, na utakuwa na miaka 5 kumaliza madarasa yako. Mipaka hii ya muda inaweza kurefushwa katika hali fulani.

AMEP hutoa njia chache tofauti za kujifunza. Unaweza kwenda madarasa ya kila siku, madarasa ya muda maalum, kujifunza nyumbani kupitia Masomo ya Mbali ya AMEP au ukafanya mazoezi na msaada wa mwalimu wa nyumbani. Huduma ya bure ya watoto inatolewa ukiwa na watoto ambao hawajafikisha umri wa kwenda shule, wakati wewe yupo darasani.

Wasiliana na laini ya masuala ya Idara ya Uhamiaji na Uraia kwa nambari 131 881, au tembelea tovuti ya AMEP ipo **www.immi.gov.au/living-in-australia/help-with-english/amep/** kufahamu ukistahiki kujifunza Kiingereza na AMEP na mahali utakapoweza kujisajili.

Huduma ya Utafsiri na Ukalimani (TIS Taifa)

Ukihitaji kuwasiliana na mtu ambaye hasemi lugha yako, TIS Taifa inaweza kutoa mkalimani kwa masaa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki. Unaweza kupigia simu TIS Taifa kwa nambari 131 450. Badala yake, idara ya serikali, biashara au huduma ya jamii unayotaka kuongea nayo inaweza kupigia TIS Taifa kwa niaba yako.

TIS Taifa inaendesha kwa msingi wa ada kwa huduma, hata hivyo, gharama ya kazi ya ukalimani inalipiwa na idara ya serikali, biashara au la kijamii unaloongea nalo.

Kama ukihitaji mkalimani wakati unapomwona daktari, unaweza kumwomba daktari yule awasiliane na TIS Taifa kutumia Simu ya Kipaumbele ya Daktari. Famasia pia inaweza kutumia wakalimani wa simu kuongea nawe. Hii ni huduma bure inayotolewa kwa madaktari na famasia.

TIS Taifa inakaribisha masuali kutoka wakazi wa kuduma na raia wanaopendezwa kutoa huduma za ukalimani kwa mpango wa mkataba kwa jamii ya Australia. Ukiwa na ustadi mzuri wa Kiingereza na angalau lugha nyingine moja, unaweza ukazingatia maombi ya kuwa mkalimani kwa mkataba wa TIS Taifa. Tafadhali wasiliana na Afisa wa Ushirikiano wa Mkalimani wa TIS Taifa, kwa 1300 132 621 kwa maelezo zaidi.

Maelezo zaidi kuhusu huduma zinazotolewa na TIS Taifa yanapatikana kutoka **www.immi.gov.au/tis**

Utafsiri kwa Kiingereza ya hati za binafsi kuhusu makazi (kwa mfano, vyeti vya kuzaliwa au ndoa, lisensi ya madereva, hati za elimu na kazi) unapatikana kwa wahamiaji wanaostahiki mnamo miaka mbili baada ya kuwasili nchini Australia, au baada kupewa makazi ya kudumu. Huduma hii ni ya bure. Kwa habari zaidi kuhusu utafsiri zinapatikana kutoka tovuti ifuatayo **www.immi.gov.au/living-in-australia/help-with-english/learn-english/client/translation_help.htm**

© COMMONWEALTH OF AUSTRALIA, 2011

Mipango ya Kiingereza ya Idara ya Elimu, Ajira na Mahusiano ya Sehemu za Kazi

Mafunzo ya lugha ya Kiingereza, kusoma na kuhesabu pia yanapatikana kupitia mipango iliyolengwa inayosimamiwa na Idara ya Elimu, Ajira na Mahusiano ya Sehemu za Kazi (DEEWR) na serikali ya jimbo na wilaya. DEEWR ina mipango 2 ya lugha ya Kiingereza, kusoma na kuhesabu inayohusiana na ajira kwa wateja wa umri wa kufanya kazi (miaka 15-64).

Wa kwanza ni Mpango wa Lugha, Kusoma na Kuhesabu (LLNP) unaotoa hadi masaa 800 ya mafunzo ya bure ya lugha, kusoma na kuhesabu yanayoelekeza kazi kwa watafuta kazi wanaostahili. LLNP inalenga kuboresha lugha ya wateja na/ama ustadi wa kusoma na kuhesabu kuwasaidia kupata ajira inayoendelea au kuingia elimu au mafunzo zaidi. Mpango pia unatoa mafunzo maalum katika Mafunzo ya Kutimizana yanayolenga kusaidia wateja wenye hali ngumu. Watu wengine wanaotafuta kazi walio na aina fulani ya viza wanaweza kukosa kustahiki mradi huu.

Wa pili ni Mpango wa Lugha ya Kiingereza na Kusoma kwa Sehemu za Kazi (WELL) ambayo inafadhili mashirika ili kuwafunza wafanyakazi Waaustralia ustadi wa lugha ya Kiingereza, kusoma na kuhesabu kuwasaidia kutimiza mahitaji ya ajira na mafunzo ya sasa na baadaye.

Serikali ya Australia pia hufadhili kusaidia mashirika ya elimu ya serikali ya jimbo na wilaya na mashirika yasiyo ya serikali kutoa masomo mfufulizo ya lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wahamiaji wapya waliowasili wa shule ya msingi na sekondari wanaostahiki chini ya Mpango wa Kiingereza kama Lugha ya Pili – Wapya waliowasili (ESL-NA). Mpango huu unalenga kuboresha mianya na matokeo ya elimu ya wanafunzi wapya waliowasili ambao hawana asili ya Kiingereza kwa kukuza uwezo wao wa lugha ya Kiingereza na kuwawezesha kuhusika kwao katika shughuli tawala za kielimu.

Wanafunzi wanaostahiki wanatazamiwa kupokea angalau miezi 6 mafunzo mfufulizo ya lugha ya Kiingereza kwa mojawapo vituo vya lugha mfufulizo au shuleni. Kila mamlaka inajukumu kupanga tathmini yake yenyewe ya mahitaji ya wanafunzi, mtalaa wa Kiingereza kama Lugha ya Pili, na kutoa mafunzo mfufulizo ya lugha ya Kiingereza.

Kwa habari zaidi:

Tovuti: www.deewr.gov.au
www.deewr.gov.au/skills/pages/default.aspx

Simu: 1300 363 079

Uraia wa Australia

Wakazi wengi wa kudumu wanaotaka kuwa waraia lazima watosheleza masharti fulani kabla kuomba uraia. Masharti haya ni pamoja na kuishi Australia kwa muda fulani na kuwa na tabia nzuri. Unapotosheleza masharti hayo waweza kufanya ombi la uraia wa Australia. Watu wengi wanaoomba uraia wa Australia pia wanahitajika kushinda mtihani wa uraia.

Maelezo kuhusu uraia wa Australia, habari zaidi kuhusu mahitaji ya makazi, vigezo vingine vya kustahiki na fomu za maombi, zinapatikana kwa tovuti ya uraia **www.citizenship.gov.au** au kupiga laini ya habari ya uraia kwa 131 880 kwa masuali katika Australia.

Habari au ushauri zaidi

Hakikisha upate nakala yako ya kijitabu cha *Kuanza Maisha Nchini Australia*. Vinapatikana kwa Kiingereza na lugha 37 za jamii, na vinapatikana kwa **www.immi.gov.au/living-in-australia/settle-in-australia/beginning-life/**

Ujumbe na ushauri wa makazi pia unapatikana kutoka ofisi za Idara ya Uhamiaji na Uraia nchini Australia na ng'ambo. Kwa habari zaidi fikia:

Idara ya Uhamiaji na Uraia
Simu: 131 881 (masuali ya jumla katika Australia)
www.immi.gov.au

Ujumbe wa kuhamia nchini Australia
www.immi.gov.au/migrants/

Ujumbe wa kuishi nchini Australia
www.immi.gov.au/living-in-australia/

Orodha ya Ofisi za Uhamiaji za Australian, za ng'ambo zipo;
www.immi.gov.au/contacts/overseas/

Kufahamu mahali pa Huduma za Makazi;
www.immi.gov.au/living-in-australia/settle-in-australia/find-help/where-to-help/

Tovuti ya Uraia
www.citizenship.gov.au

Maelezo zaidi

Dharura zinazotisha Maisha
(Wazima Moto, Polisi, Ambulensi) – Masaa 24
Simu: 000

Huduma ya Utafsiri na Ukalimani (TIS Taifa)
Simu: 131 450
www.immi.gov.au/tis/

Huduma ya Habari za Mikoa ya Serikali ya Australia
Simu: 1800 026 222
www.regionalaustralia.gov.au

Tovuti ya Habari za Kutambua Ustadi wa Australia
www.immi.gov.au/asri

Kutambua Utaalamu Australia
Simu: 1300 360 992
www.deewr.gov.au/tra

Tovuti ya Serikali ya Australia
www.australia.gov.au

Ukarasa wa nyumbani **www.immi.gov.au**

Laini ya masuali ya jumla Piga simu **131 881** kati masaa ya ofisi katika Australia kuongea na opereta (habari zilizorekodiwa zinapatikana nje masaa hayo). Ukiwepo nje Australia, uwasiliane na ubalozi wa Australia wa karibu sana ya kwako.

© COMMONWEALTH OF AUSTRALIA, 2011